

# WETCU 2018 LTD

REG NO.

5483

Telegraph: WETCU LTD  
Tel: +255 262605270, +255262606125  
Fax: +25526260 5071  
E-Mail: [wetcultd@gmail.com](mailto:wetcultd@gmail.com)



Coronation Road,  
P. O. Box 64,  
Tabora, Tanzania,  
East Africa.

---

22/10/2020

## TANGAZO LA KAZI

CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA WETCU 2018 LTD CHENYE MAKAO MAKUU YAKE MJINI  
TABORA MANISPAA KINATANGAZA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO;

### 1. AFISA WA SHERIA (LEGAL ADVISOR) – NAFASI 1

#### Sifa za Kitaaluma

Shahada ya sheria kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali, awe na Uzoefu usiopungua miaka mitatu (3) katika masuala yahasuyo sheria katika mashauri ya jinai na madai katika taasisi binafsi na taaasisi za umma.

#### Kazi na Majukumu

Kazi na majukumu ya Afisa wa sheria yatakuwa kama ifuatavyo:

- (a) Kuhakikisha kuwa shughuli na uendeshwaji wa Bodi ya WETCU 2018 LTD havikiniani na matakwa ya sheria iliyoanziasha WETCU 2018 LTD.
- (b) Kuikumbusha Bodi ya WETCU 2018 LTD kutenda kwa kuzingatia kama inavyotakiwa kufuata matakwa ya kisheria.
- (c) Kuwa Mshauri Mkuu wa Meneja Mkuu katika masuala yote yahasuyo sheria na katika kuishauri Bodi na masuala yahasuyo Mkutano Mkuu.

- (d) Kusimamia mashauri yote yanayoihusu WETCU 2018 LTD ikiwa ni pamoja na kuandaa au kufanya marejeo ya nyaraka zote za kisheria za WETCU 2018 LTD kama vile Mikataba ya pango, n.k. Kurejea taarifa za kaguzi za Menejimenti kwa wateja wakubwa na kuainisha kama kuna athari yoyote ya kisheria.
- (e) Kufanyia marekebisho mahususi Masharti au sheria ndogondogo za WETCU 2018 LTD juu ya kanuni na mabadiliko ya mapendekezo ili yaende sambamba na mabadiliko ya mahitaji ya sheria ya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013, na mazingira ya uendeshaji wa WETCU 2018 LTD.
- (f) Kusimamia masuala ya kisheria na kumbukumbu, na nyaraka za kisheria za WETCU 2018 LTD.
- (g) Kupokea na kuandaa taarifa ya kulipwa na malipo ya gharama za kesi katika mahakama.
- (h) Kuaanda taarifa ya mwezi kuhusu mashauri yaliyofanyika.
- (i) Kutekeleza na kushiriki katika kupanga na kuridhia Mikataba ya kiutendaji yenye taarifa za moja kwa moja.

## **2. AFISA UGANI (LEAF MAN) – NAFASI 2**

### **Sifa za Kitaaluma**

Awe na Cheti au Stashahada ya Sayansi ya kilimo (Agriculture general), kutoka chuo cha kilimo kinachotambuliwa na serikali, awe na uzoefu usiopungua miaka 3 kazini katika shughuli zihusuzo kutoa elimu ugani kwa wakulima hususani zao la tumbaku katika masuala ya Ushirika.

### **Kazi na Majukumu**

- (a) Kupanga na kutoa tathimini ya maendeleo ya wakulima wa vyama vya Msingi vya WETCU 2018 LTD.
- (b) Kutoa ushauri kwa wakulima katika vyama vya msingi juu ya namna bora ya kulima kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo.

- (c) Kubuni mbinu bora za kuwafikia wakulima wote ili kuwawezesha kulima kwa tija na kupata mazao bora.
- (d) Kusimamia masoko ya tumbaku katika vituo tumbaku inakouziwa.
- (e) Kushauri namna bora ya usambazaji wa pembejeo kwa wakulima ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.
- (f) Kuhamasisha na kushauri wakulima ili kulima kwa kuzingatia kanuni bora za uzalishaji.
- (g) Kuendesha mafunzo kwa mifano ya mashamba darasa juu ya kilimo bora kwa wakulima katika vyama vya msingi.
- (h) Kutoa taarifa kwa wakati juu ya shughuli za uzalishaji na uendeshaji wa masoko kwa Meneja Shughuli na vifaa kwa hatua zaidi.
- (i) Kutekeleza na kushiriki katika kupanga na kuridhia Makubaliano ya kiutendaji yenye taarifa za moja kwa moja.
- (j) Kutekeleza kazi au majukumu mengine kama itakavyoelekezwa na Meneja shughuli

**MUHIMU :**

Mshahara kwa nafasi zote za kazi utazingatia Ngazi za Chama Kikuu cha Ushirika WETCU 2018 LTD.

Tuma maombi yakiambatana na vyeti vya shule, taaluma na Maelezo binafsi, maombi yatamwe ndani ya siku kumi na nne (14), tangu kutolewa kwa tangazo hili.

MENEJA MKUU  
WETCU 2018 LTD  
S. L. P 64  
TABORA

Email / barua pepe : [wetcultd@gmail.com](mailto:wetcultd@gmail.com)